AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430
**MUHTASARI WA HUKUMU**

**RASHIDI ROMANI NYERERE DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 023/2018**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**TAREHE 13 NOVEMBA 2024**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, tarehe 13 Novemba 2024**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama), leo, imetoa Hukumu katika kesi ya *Rashidi Romani Nyerere dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

Rashidi Romani Nyerere (Mleta Maombi) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi). Wakati wa kuwasilisha Maombi haya, alikuwa amefungwa katika Gereza Kuu la Ruanda mkoani Mbeya, baada ya kusikilizwa kesi na kukutwa na hatia ya mauaji na akahukumiwa kifo kwa kunyongwa. Mleta Maombi alidai kwamba Mjibu Maombi alikiuka haki yake ya kusikilizwa kwa haki na haki yake ya utu kwa kumhukumu kwa misingi ya kukiri makosa na ushahidi uliopatikana kinyume cha sheria, na kwa kumweka kwenye mahabusu ya polisi kwa muda mrefu kuliko inavyoruhusiwa kisheria. Mleta Maombi alidai zaidi kwamba aliteswa alipokuwa kwenye mahabusu ya polisi. Kwa hivyo, alitaka apewe fidia ili kufidia ukiukaji huu unaodaiwa kufanywa.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki), Mahakama iliona kwamba ilipaswa kwanza kuamua endapo ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Maombi hayo. Katika suala hili, Mjibu Maombi aliibua pingamizi kuhusu mamlaka halisi ya Mahakama, akidai kwamba Mahakama haikuwa na uwezo wa kufuta hukumu zilizotolewa na mahakama za ndani wala Mahakama hii isingeweza kukaa kama Mahakama ya Rufaa, ambayo inaweza kuunga mkono au kubatilisha hukumu za mahakama za ndani. Hata hivyo, Mahakama hii, huku ikikiri kwamba si mahakama ya rufaa kuhusiana na maamuzi ya mahakama za ndani, iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya kuamua endapo uendeshaji wa kesi katika mahakama za ndani ulifanywa kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa katika Mkataba na vyombo vingine vya haki za binadamu vilivyoidhinishwa na Mjibu Maombi. Aidha, Mahakama iliona kwamba ina uwezo wa kutoa amri zinazofaa ili kutoa haki kuhusu ukiukaji wa haki za binadamu, kwa hivyo, ina uwezo wa kuamuru hukumu ifutwe pale ambapo amri hiyo ni suluhisho linalofaa.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Mjibu Maombi, hata hivyo, Mahakama ilivichunguza. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka binafsi kwani, tarehe 29 Machi 2010, Mjibu Maombi iliweka Azimio lililotolewa chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki, ambacho kinaruhusu

watu binafsi kuwasilisha maombi dhidi ya Mjibu Maombi kulingana na Kifungu cha 5(3) cha Itifaki. Mahakama ilisisitiza kwamba Mjibu Maombi kuondoa Azimio hilo, mnamo tarehe 21 Novemba 2019, hakukuathiri Maombi haya kwani uondoaji huo ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 22 Novemba 2020, ambayo ilikuwa tarehe baada ya Maombi haya kuwasilishwa, mnamo tarehe 5 Desemba 2018.

Mahakama pia iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa ulitokea baada ya Mjibu Maombi kuwa mhusika wa Itifaki. Mwisho, ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, ikizingatiwa kuwa ukweli wa jambo hilo ulitokea ndani ya eneo la Mleta Maombi.

Mahakama iliona kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki, Mahakama lazima iamue kuhusu ukubalifu wa kesi zilizowasilishwa mbele yake. Katika suala hili, Mjibu Maombi aliweka mapingamizi mawili, ambayo yalikuwa ni kwamba Mleta Maombi alikuwa hajakamilisha taratibu za ndani na kwamba Maombi hayakuwasilishwa ndani ya muda unaofaa. Kuhusu kukamilisha taratibu za ndani, Mjibu Maombi aliwasilisha kwamba madai ya Mleta Maombi kuhusu mateso hayakuwasilishwa mbele ya mahakama za ndani. Aidha, Mjibu Maombi aliwasilisha kwamba Mleta Maombi alishindwa kuomba uamuzi wa Mahakama ya Rufaa urejewe na uhakikiwe, kabla ya kuifikia Mahakama hii. Kuhusu pingamizi la Maombi kuwa limewasilishwa ndani ya muda muafaka, Mjibu Maombi aliwasilisha kwamba miaka mitatu na miezi mitatu ambayo ilitumika kuwasilisha Maombi haukuwa muda faafu.

Mahakama ilitupilia mbali pingamizi la Mjibu Maombi kuhusu kukamilisha taratibu za ndani, kwa sababu Mleta Maombi hakutakiwa kuomba uamuzi wa Mahakama ya Rufaa upitiwe upya, kwani huu ni utaratibu usio wa kawaida. Aidha, Mahakama iliona kwamba Mleta Maombi alikuwa amekamilisha taratibu za ndani kuhusiana na madai ya mateso na ushahidi uliopatikana kinyume cha sheria. Kuhusu madai ya kuwekwa kizuizini polisi kwa muda mrefu, Mahakama iliona kwamba Mleta Maombi alikuwa hajakamilisha taratibu za ndani na kwa hivyo, iliona madai haya hayakubaliki. Tena Mahakama ilitupilia mbali pingamizi la Maombi kuwa yamewasilishwa ndani ya muda mwafaka, kwa sababu kwamba miaka mitatu na miezi mitatu ambayo ilitumika kuwasilisha Maombi ilikuwa ni muda unaofaa, ikizingatiwa kwamba Mleta Maombi si mwanasheria, na kwamba aliwasilisha Maombi wakati akiwa gerezani na akiwa hana msaada wa wakili. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba, isipokuwa madai ya Mleta Maombi yanayohusiana na kuwekwa kizuizini polisi kwa muda mrefu, Maombi yalizingatia Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama, pamoja na Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama.

Ingawa masharti mengine ya ukubalifu hayakupingwa na Mjibu Maombi, hata hivyo, Mahakama iliyachunguza. Kwa hivyo, Mahakama ilibainisha kuwa Mleta Maombi alikuwa ametambuliwa kwa udhahiri kwa jina katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama. Iliona pia kwamba madai ya Mleta

Maombi yalilenga kulinda haki zake kulingana na Kifungu cha 3(h) cha malengo ya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Maombi yalizingatia Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama.

Aidha, Mahakama ilibaini kwamba lugha iliyotumika katika Maombi haikuwa ya dharau au ya matusi kwa Mjibu Maombi au taasisi zake katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za Mahakama. Maombi haya pia hayakutokana tu na habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari, kwani yalitokana na nyaraka za kisheria, katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Maombi haya yalikuwa yametimiza masharti yote ya ukubalifu.

Kuhusu uzingatiaji wa sheria wa kesi hiyo, Mahakama iliangalia endapo Mjibu Maombi alikiuka haki za Mleta Maombi zilizo chini ya Kifungu cha 1, 4, 5, na 7 cha Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (Mkataba).

Kuhusiana na Kifungu cha 4 cha Mkataba kuhusu haki ya kuishi, Mahakama ilibainisha kuwa Mleta Maombi hakutoa maelezo kuhusu jinsi kifungu hiki kilivyokiukwa. Hata hivyo, Mahakama, ilizingatia ikiwa kifungu hiki kilikiukwa kwa matumizi ya lazima ya hukumu ya kifo. Kulingana na busara yake ya kisheria, Mahakama iliona kwamba kutolewa kwa adhabu ya kifo ya lazima hakukumruhusu afisa wa mahakama kutumia busara ya kisheria. Kwa hivyo, haki ya Mleta Maombi ya kuishi ilikuwa imekiukwa.

Kuhusiana na Kifungu cha 5 cha Mkataba kuhusu haki ya utu, Mahakama iliangalia endapo kifungu hiki kilikiukwa, kulingana na madai ya mateso na ya kulazimishwa kukiri hadharani. Kwa hiari yake, Mahakama pia iliangalia endapo kifungu hiki kilikiukwa kulingana na kutolewa kwa lazima kwa hukumu ya kifo na njia ya kutekeleza hukumu ya kifo, yaani kwa kunyongwa. Mahakama iliona kwamba Mleta Maombi alikuwa hajateswa akiwa chini ya ulinzi wa polisi na, kwa hivyo, haki yake ya utu haikuwa imekiukwa, kwa msingi wa kuteswa. Hata hivyo, Mahakama ilienda mbali zaidi na kusisitiza uamuzi wake wa kisheria kwamba utekelezaji wa hukumu ya kifo kwa kunyongwa ni ukiukaji wa haki ya utu. Kwa hivyo, kwa msingi huu, Mahakama iliona kwamba haki ya utu ya Mleta Maombi ilikuwa imekiukwa.

Kuhusiana na madai ya ukiukaji wa Kifungu cha 1 na cha 7 cha Mkataba, Mahakama iliona kwamba jinsi kesi za ndani zilivyoendeshwa zilifuata viwango vya kimataifa, na kwa hivyo madai ya ukiukaji wa haki ya kusikilizwa kwa haki, inayolindwa chini ya Kifungu cha 7(1) cha Mkataba, yalitupiliwa mbali. Mahakama iliendelea kusema kwamba madai ya Mleta Maombi ya ukiukaji wa Kifungu cha 1 cha Mkataba, kwa sababu ya yeye kuteswa na ukosefu wa haki katika kesi zilizo mbele ya mahakama za ndani, hayakuwa na ushahidi.

Mahakama iliendelea kusema kwamba kutokana na ukiukaji ulioabainishwa wa Kifungu cha 4 na 5 cha Mkataba, kulingana na kudumisha hukumu ya lazima ya kifo na njia ya kutekeleza hukumu ya kifo, Kifungu cha 1 cha Mkataba kilikuwa kimekiukwa pia.

Mahakama, baada ya kubaini ukiukaji wa Kifungu cha 1, 4, na 5 cha Mkataba, ilimpa Mleta Maombi kiasi cha Shilingi za Tanzania Laki Tatu (TZS 300,000), ili kufidia hasara ya kimaadili iliyosababishwa na Mleta Maombi, kutokana na kutolewa kwa adhabu ya kifo kwa lazima.

Aidha, Mahakama iliamuru Mjibu Maombi achukue hatua zote muhimu, ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya kupokea taarifa ya Hukumu, kuondoa kwenye sheria zake utoaji wa hukumu ya kifo ya lazima; kuchukua hatua zote muhimu kuondoa kwenye sheria zake adhabu ya kunyongwa, kama njia ya kutekeleza hukumu ya kifo, ndani ya miezi sita baada ya kupokea taarifa ya Hukumu hii; achapisha Hukumu hii kwenye tovuti za Mahakama, na Wizara ya Katiba na Sheria, ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu kupokea taarifa na kuhakikisha kuwa hati ya hukumu inapatikana kwa angalau mwaka mmoja baada ya tarehe ya kuchapishwa. Mjibu Maombi pia aliamriwa achukue hatua zote muhimu ili kupitie tena kesi ya Mleta Maombi kuhusu hukumu, kupitia utaratibu ambao unaruhusu kutumia busara ya mahakama.

Mahakama pia iliamuru Mjibu Maombi atoe ripoti za mara kwa mara kuhusu utekelezaji wake wa Hukumu, na kutoa ripoti kuhusu hatua ambazo imechukua kutekeleza Hukumu ndani ya miezi sita tangu tarehe ya kupokea taarifa.

Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 70(3) ya Kanuni za Mahakama, Jaji Blaise Tchikaya na Jaji Dumisa B. Ntsebeza walitoa Maazimio kuhusu suala la adhabu ya kifo.

**Maelezo zaidi**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, inaweza kupatikana kwenye tovuti kwenye: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0232018.

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na*

*utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*